| **Mifano ya viashiria vilivyotengenezwa na jamii kama nguzo za eneo la hifadhi ya jadi**<br><br>Imetafsiriwa na: Jumapili Chenga<br>Mhariri: Casian Sianga<br>Septemba, 2023 | |
|---|---|
| **Kiashiria mfano** | **Tafakari juu ya ubora wa kiashiria** |
| **Nguzo za Eneo la hifadhi ya jadi: Uadilifu na nguvu ya jamii ya wamiliki** | |
| Hisia ya utambulisho, muunganiko, mshikamano kwa 'kila mmoja' na 'kuwa sehemu ya jamii | Kwa ulinganifu inaweza kutathminiwa kwa urahisi kwa kuzingatia vikundi, mahojiano, au majadiliano katika hali ya kawaida mikusanyiko ya jamii, ingawa majibu ni binafsi |
| Idadi ya shughuli zilizoamuliwa na kufanywa kwa pamoja na kwa mafanikio na jamii katika mwaka fulani (kwa mfano kurekebisha bwawa dogo la maji, kujenga shule ya mtaa, kupanda tena mikoko) | Kiashiria halali… lakini siyo sahihi sana kwa sababu shughuli hizo zinaweza kutakiwa au kuletwa na mazingira ya nje |
| Uwezo wa jamii kuzungumza kwa sauti moja | Kiashiria halali… lakini ni vigumu kukitathmini |
| Kujirudia mara kwa mara, mahudhurio, na shauku kubwa iliyoonyeshwa kwa ajili ya matukio ya kitamaduni ya jamii na sherehe | Kwa ulinganifu, ni rahisi kutathmini, lakini siyo sahihi sana kwasababu watu wanaweza kushiriki kwa sababu zisizohusiana na hisia zao za mshikamano na jamii |
| Idadi ya watu, kutoka familia mbalimbali na makundi, yanayosaidiana wakati wa shida | Inaweza kuwa kiashiria halali ikiwa ni muhimu kwa kanuni za jamii, lakini huenda zisiwe sahihi sana na inaweza kuwa ngumu kutathmini |
| **Nguzo za eneo la hifadhi ya jadi: Muunganiko kati ya jamii na eneo lake** | |
| Idadi ya siku ambazo watu walifanya kazi kama jamii kwa kujitolea katika eneo la hifadhi ya jadi kwa wakati fulani | Kiashiria kizuri ambacho kinaweza kufuatwa kila mwezi; inawezekana pia kukigawanya kwa kijiji, kwa msimu, n.k. |
| Asilimia ya watu katika jamii wanaoweza kutaja na kuelezea angalau vipengele 10 tofauti au vipengele vidogo ndani ya eneo la hifadhi ya jadi | Kiashiria kizuri, na siyo kigumu sana kukipima, lakini siyo wazi jinsi gani kinaweza kuwa halali – maana yake ikiwa ni kupima kile kinachokusudiwa kupima |
| Idadi/asilimia ya watu kutoka katika vikundi vyote vya kijamii vinavyoshiriki katika juhudi za 'linda' eneo la hifadhi ya jadi wakati liko katika tishio | Kiashiria halali kabisa, na siyo kigumu sana kukipima. Hata hivyo huenda kisiwe sahihi kabisa, kwani ushiriki unaweza kutofautiana kulingana na mambo mbalimbali (ukubwa wa tishio, upatikanaji wa hatua za majibu, nk) |
| Kujirudia mara kwa mara, mahudhurio, na kujieleza kwa shauku kubwa kwa ajili ya matukio ya kitamaduni ya jamii na sherehe maalum kwa eneo la hifadhi ya jadi | Kiulinganifu ni rahisi kutathmini, lakini siyo sahihi kabisa kwa vile watu wanaweza kushiriki kwa sababu mbalimbali |
| Kujirudia mara kwa mara, mahudhurio, na shauku kubwa iliyoonyeshwa ya fursa za kujifunza kati ya vizazi kuhusu eneo la hifadhi | Kiulinganifu ni rahisi kutathmini, labda siyo sahihi sana kwa vile kama watu wanaweza kushiriki kwa sababu mbalimbali |

| | |
|---|---|
| ya jadi, kwa mfano mikutano kati ya wazee na vijana | |
| Hisia ya uhusiano na eneo la hifadhi ya jadi | Kinaweza kiulinganifu kutathminiwa kwa urahisi kwa vikundi, mahojiano, au majadiliano katika mikusanyiko ya kawaida ya jamii, ingawa majibu ni binafsi |
| **Nguzo za eneo la hifadhi ya jadi: Utendaji wa taasisi ya utawala** | |
| Idadi na ukubwa wa ukiukaji wa sheria za eneo la hifadhi ya jadi katika mwaka fulani | Si sahihi wala maalum kwa kitu kimoja na inaweza kuwa vigumu kutafsiri (kwa mfano ni ukiukwaji unaoongezeka kwa sababu utawala unadhoofika, au kwa sababu ufuatiliaji umekuwa bora? |
| Idadi ya migogoro mikubwa ya ndani ya jamii inayohusiana na matumizi ya maliasili katika eneo la hifadhi ya jadi | Kiashiria halali cha matokeo, ingawa siyo sahihi sana au maalum kwa kitu kimoja. Kinaweza kuimarishwa kwa kuunganishwa na habari kuhusu chanzo cha migogoro. Je, inatokea kwa sababu ya juhudi za kuboresha utawala? Au kwa sababu utawala unadhoofika? |
| Kimeonyesha uwezo wa kufanya maamuzi katika hali ya msongo | Kiashiria halali… lakini siyo sahihi sana na wakati mwingine ni vigumu kukitathmini |
| Kiwango ambacho au urahisi ambao wanajamii wanaweza kupata taarifa (kuweka kumbukumbu, maelezo) kuhusu eneo la hifadhi ya jadi kutoka katika taasisi yake ya uongozi | Kinaweza kiulinganifu kutathminiwa kwa urahisi kwa vikundi, mahojiano, au majadiliano katika mikusanyiko ya kawaida ya jamii, ingawa majibu ni binafsi |
| Kiwango ambacho taasisi imeweza kwa ufanisi kukabiliana na matishio na matatizo yanayojitokeza kwenye eneo la hifadhi ya jadi kwa wakati na muda fulani | Kiashiria halali, kinaweza kiulinganifu kutathminiwa kwa urahisi kwa vikundi, mahojiano, au majadiliano katika mikusanyiko ya kawaida ya jamii, ingawa majibu ni binafsi |
| Kiwango cha mtazamo kilichoonyeshwa cha uhalali unaotambulika wa taasisi ya uongozi | Kinaweza kiulinganifu kutathminiwa kwa urahisi kwa vikundi, mahojiano, au majadiliano katika mikusanyiko ya kawaida ya jamii, ingawa majibu ni binafsi |
| Ufadhili uliotafutwa na taasisi inayosimamia kusaidia shughuli za ufuatiliaji zinazoendelea | Kiashiria halali na rahisi kutathmini, lakini inategemea sana mazingira ya nje ya udhibiti wa jamii |
| Idadi ya watu wanaoshiriki kikamilifu katika kazi za taasisi ya utawala | Kiulinganifu, rahisi kutathmini, hasa ikiwa itifaki ya ufuatiliaji iko wazi |
| **Nguzo ya eneo la hifadhi ya jadi: Afya ya ikolojia na uadilifu wa eneo** | |
| Ubora na wingi wa samaki wanaovuliwa kutathminiwa katika hali ya umakini, katika maeneo maalum katika eneo la hifadhi ya jadi, kwa nyakati maalum katika kalenda ya uvuvi na kwa kutumia zana za kawaida zilizowekwa maalum kwa madhumuni hayo tu | Jozi bora kabisa, ya viashiria iliyokamilika - ya kutegemewa, kamilifu na maalum ... lakini siyo rahisi au yenye gharama nafuu kuanzisha. Kufuatilia hili kunahitaji rasilimali za kujitoa |
| Ubora na wingi wa mimea inayopatikana mahali hapo pekee ambayo ni muhimu kwa jamii | Kiashiria halali ikiwa itifaki itawekwa kwa uangalifu na kufuatwa |

| | |
|---|---|
| Mara ngapi mnyama aliye hatarini kutoweka ameonekana katika hali iliyodhibitiwa | Kiashiria halali ikiwa itifaki imetengenezwa kwa uangalifu na kufuatwa |
| Mitiririko ya ubora wa udongo, ubora wa maji, ubora wa hewa na/au ubora wa misitu, nyanda za malisho, miamba ya matumbawe na viashirio vingine vya kiikolojia vilivyopimwa katika hali zilizodhibitiwa | Kiashiria halali ikiwa itifaki imetengenezwa kwa uangalifu na kufuatwa na kuzingatia kuingiliwa na mambo yaliyo nje |
| **Nguzo ya eneo la hifadhi ya jadi: Kipato cha kujikimu na maisha na ustawi wa jamii** | |
| Wastani wa mzunguko wa kila mwezi wa kula vizuri chakula bora kati ya familia zote kijijini | Kina maana sana lakini inaweza kuwa ngumu kuamua kama inatathminiwa kwa kufanya mahojiano na kaya zote. Chaguo rahisi zaidi linaweza kuwa kuunda makundi lengwa au kusaili sehemu ndogo lakini wakilishi ya familia ili kufichua mienendo yenye maana. |
| Mitiririko ya uhamiaji wa wanaoingia ndani na uhamiaji wa wanaotoka nje wa wanakijiji/wanajamii | Kina maana lakini ngumu kuamua bila kuwa na utata, na mara nyingi siyo sahihi sana kwa sababu zile harakati zinaweza kutokea kwa kwasababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuongezeka na kupungua kwa mali na fursa za kujikimu. |
| Viashiria vya afya ya jamii kwa ujumla na hali ya lishe hasa ya mtoto | Kiashiria cha maana lakini kinahitaji usaidizi wa kitaalam ili kutengeneza itifaki ya kipimo. Inaweza pia kuwa vigumu kujua ni kiasi gani eneo la hifadhi ya jadi linaathiri mabadiliko yoyote katika afya ya jamii na/au lishe ya mtoto |
| Asilimia ya watu wanaojisikia kwa kiasi kikubwa au kikamilifu kuridhika na maisha yao | Kiashiria halali, lakini kinaweza kuwa vigumu kutathmini na upendeleo unaweza kuletwa kwa urahisi katika itifaki ya kipimo. Inaweza pia kuwa vigumu kujua ni kiasi gani eneo la hifadhi ya jadi hasa linathiri hali hii ya ustawi |
| **Viashiria vipana kufunua nguvu kuu na udhaifu wa eneo la hifadhi ya jadi** | |
| Ufahamu wa kijamii juu eneo la hifadhi ya jadi katika jamii ya wamiliki na kwingineko | Halali na muhimu sana, lakini inahitaji juhudi za kujitoa kufanya tathmini |
| Upatikanaji wa rasilimali watu na fedha kwa kusaidia shughuli za ufuatiliaji | Halali, muhimu sana na kiulinganifu ni rahisi kutathmini |
| Kutambuliwa na mamlaka za serikali (manispaa, mkoa, wawakilishi wa serikali kuu; mahakama) | Halali, muhimu sana na kiulinganifu ni rahisi kutathmini |